# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA KUMI NA TATU

**15 FEBRUARI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### KIKAO CHA KUMI NA TATU– TAREHE 15 FEBRUARI, 2024

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA FEDHA:

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha – Mapitio ya Nusu Mwaka 2023/2024 *(Monetary Policy Statement - Mid - Year Review 2023/2024).*

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**211. MHESHIMIWA AMANDUS JULIUS CHINGUILE (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali italigawa Jimbo la Nachingwea.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**212. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kulipa fedha za madaraka kwa Waganga Wafawidhi wa Vituo vya Afya na Zahanati nchini.

**213. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Lang'ata – Mwanga.

**214. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kujenga Vituo vya Afya kwenye Kata za pembezoni mwa Mkoa wa Simiyu.

**WIZARA YA UJENZI:**

**215. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, nini kinakwamisha ujenzi wa Barabara ya Same – Kisiwani – Ndungu hadi Mkomazi licha ya kutengewa fedha miaka minne mfululizo.

## WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

**216. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itaboresha Uwanja wa Michezo katika eneo la Polisi Himo.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**217. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani kwa Watumishi wanaokaimu nafasi kwa muda mrefu katika Vyuo vya FETA ikiwemo Mtwara.

**218. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaajiri Maafisa Mifugo katika kila Kata ili kuwasaidia Wafugaji.

**WIZARA YA KILIMO:**

**219. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuongeza Uzalishaji wa Zao la Pareto.

**220. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini skimu za umwagiliaji za Katengara, Muhwazi, Gwanumbu na Ruhwiti katika Wilaya ya Kakonko zitakarabatiwa.

**221. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya Umwagiliaji katika Skimu ya Dongobeshi kufuatia kukamilika ujenzi wa Bwawa la Dongobeshi.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**222. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanza ujenzi wa kipande cha Reli ya TAZARA kutoka Tunduma hadi Bandari ya Kasanga.

**WIZARA YA AFYA:**

**223. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, tafiti zipi ambazo Taasisi za Tiba Asili zimekamilisha na kuweza kuwa suluhisho la maradhi mbalimbali kama Tiba Mbadala.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**224. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni kweli kuna Wazee wanaodai haki zao kutokana na ushiriki wao kwenye Vita vya Dunia au Jeshi la KAR.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 (*The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024.*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024.*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024.*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024.*

## V. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**DODOMA**
**15 FEBRUARI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**